MKUTANO WA MKUU WA CHUO, PROF. SHADRACK S. MWAKALILA, NA WAFANYAKAZI WA CHUO CHA KUMBUKUMBU YA MWALIMU NYERERE,
KAMPASI YA KIVUKONI, DAR ES SALAAM
JUMANNE, TAREHE 12 DISEMBA, 2023

Ndugu Watumishi wenzangu,

Awali ya yote Napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi MUNGU kwa kutuwezesha wote kushiriki katika mkutano huu mhimu kwa ajili ya ustawi wa Chuo chetu cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere na Taifa kwa ujumla. Aidha nitumie nafasi hii kuwakaribisha watumishi wote wapya ambao wameajiriwa hivi karibuni. Pia nawapongeza watumishi wote kwa kazi nzuri na uwajibikaji wa kila mmoja sehemu yake kazi.

Ndugu Watumishi wenzangu,

Lengo kuu la mkutano huu ni pamoja na yafuatayo:

1) Kuwapa taarifa fupi kuhusu mafanikio ya Chuo na Changamoto zake
2) Kukumbushana wajibu wetu kama watumishi wa umma
3) Kujibu hoja mbalimbali za watumishi na kuzitolea ufafanuzi.

1. MAFANIKIO YA CHUO NA CHANGAMOTO

Katika mwaka wa fedha 2022-2023, chuo kimepata mafaniko makubwa katika kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:

1.1Maboresho ya Miundombinu ya Kampasi ya Kivukoni,

Katika Kampasi ya Kivukoni miundombinu mbalimbali ya kufundishia na kujifunzia imeboreshwa ili kuongeza ubora wa mafunzo, ikiwa ni pamoja na kufunga vifaa mbalimbali vya kufundishia katika kumbi za mihadhara. Kwa sasa

Kampasi ya Kivukoni ina miundombinu inayoboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia ikiwa ni pamoja na madarasa na kumbi za mihadhara ambazo zimeboreshwa sana. Aidha mradi wa ujenzi wa jengo litakalo kuwa na Ukumbi wa Mihadhara wenye uwezo wa kutumiwa na wanafunzi 1000 pamoja na Maktaba itakayo kuwa na uwezo wa kutumiwa na wanafunzi 2500 kwa wakati mmoja unaendelea vizuri.

Ukarabati uliofanyika - Ukarabati wa miundombinu ya mifumo ya maji safi na maji taka, ukarabati wa mifumo ya umeme, ukarabati wa chumba cha kuhifadhia mifumo ya Kompyuta (Server room) na ukarabati wa maliwato. Bado kazi inaendelea ya ufungaji wa umeme wa Jenereta kwenye jengo la vitivo vya sanaa na sayansi za jamii na kitivo cha elimu pamoja na ukarabati wa Tanki kuu la maji lililopo eneo la Mikoroshini. Uunganishwaji wa maji ya DAWASA kwenye nyumba za watumishi umefanyika, Awamu ya kwanza nyumba kumi, awamu ya pili nyumba 17. Ukarabati wa Ukumbi wa Kibweta. Huduma ya ulinzi imeboreshwa, kwa sasa tuna Kampuni mpya ya Ulinzi ya SUMA JKT

1.2 Kuongeza Programme za Mafunzo katika ngazi ya Shahada ya Umahiri

Programme mbili za mafunzo ngazi ya Shahada ya Umahiri zimeongezeka katika kipindi cha 2022/2023 na kufikia programme tatu kwa sasa kama ifuatavyo:

1) Shahada ya Umahiri katika fani ya Usimamizi wa Rasili Mali Watu
2) Shahada ya Umahiri katika fani ya Uongozi na Sayansi ya Utawala
3) Shahada ya Umahiri katika fani ya Jinsia na Maendeleo

1.3 Kuongeza miradi ya tafiti katika fani mbalimbali za kitaaluma

Katika mwaka 2022/2023, Chuo kilitenga bajeti Sh 80,000,000/= kwa ajili ya kuwawezesha wahadhiri kufanya tafiti mbalimbali zenye maslahi kwa Chuo na taifa

kwa ujumla. Aidha, mwaka 2023/2024 Chuo kimeongeza bajeti ya utafiti hadi Sh 100,000,000/= kwa ajili ya kuwezesha wahadhiri kufanya tafiti mbalimbali.

1.4 Kuongeza Udahili wa Wanafunzi katika Kampasi zote

- Kivukoni udahili umeogezeka kutoka wanafunzi 14,238 mwaka 2022/2023 hadi 14,457 mwaka 2023/2024. Ongezeko la wanafunzi ni ishara kuwa wanafunzi na wazazi wana imani na Chuo hiki na mategemeo makubwa ya kupata wahitimu walioelimika na wenye maarifa na ujuzi wa kuchangia kwa haraka maendeleo yao na Taifa kwa ujumla.

1.5Kuongeza Wahitimu katika Kampasi zote

- Kampasi ya Kivukoni kutoka wahitimu wameongezeka kutoka wahitimu 5480 katika Mahafali ya 17 (2022) hadi kufikia wahitimu 5499 katika Mahafali haya ya 18 (2023 ambao walitunukiwa vyeti katika ngazi ya Astashahada ya Awali, Astashahada, Stashahada, Shahada na Shahada ya Umahiri.

1.6 Kuongeza Wahadhiri wenye Shahada ya Uzamivu (PhD)

Chuo kimewezesha Wahadhiri 58 kwenda kwenye mafunzo kwa ngazi mbalimbali za masomo ikiwemo Shahada ya Uzamivu (47), Shahada ya Umahiri (11), Shahada ya Awali. Hivyo, idadi ya Wahadhiri wenye shahada ya uzamivu (PhD) imeongezeka hadi wahadhiri zaidi ya 50 waliopo Chuoni.

1.7 Kuongezeka kwa Idadi ya watumishi

Katika kipindi cha kuanzia July 2023 hadi Disemba 2023 Idadi ya watumishi imeongezeka kutoka watumishi 305 hadi kufikia watumishi 334. Ongezeko hilo limetokana na Ajira mpya 14 na watumishi waliohamia 15. Idadi hiyo inatarajiwa

kuongezeka tena mwishoni mwa mwezi huu wa Disemba 2023 kwani watumishi wapya 11 wameshaitwa kuripoti kazini. Hata hivyo Chuo kinaendelea na mchakato wa kuajiri watumishi wengine wapya 53.

1.8. Idadi ya watumishi waliopandishwa vyeo

Watumishi waliopanda vyeo 45 (Wanataaluma 30 waendeshaji 15), Kwa sasa Chuo kina Maprofesa 2, Wahadhiri waandamizi 15, Wahadhiri 40.

1.9 Idadi ya watumishi waliopo masomoni

Watumishi 62 wanasoma masomo ya muda mrefu (Wanataaluma 58 na Waendeshaji 4). Wanaosoma Shahada ya Uzamivu wapo 47, Shahada ya Umahiri 14 na Shahada ya awali ni mmoja 1.

Aidha, Chuo kimetenga bajeti ya kuwalipia gharama za tafiti pamoja na ada za masomo watumishi waliopo Masomoni.

1.10. Changamoto na Mkakati wa kuzitatua

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Chuo kina changamoto kubwa zifuatazo:

1) Bajeti ya Chuo inategemea sana mapato ya ndani ambayo yanatokana na malipo ya Ada za wanafunzi. Mkakati ni kuongeza vyanzo vingine vya mapato ya ndani ikiwa ni pamoja na mapato yanayotokana na miradi tafiti za kitaaluma pamoja na Shauri za kitaaluma katika sekta za umma na binafsi.

2) Upungufu wa wafanyakazi kwa mujibu wa mahitaji halisi ya chuo. Mkakati ni kuendelea kuomba vibali vya ajira kulingana na mahitaji ya Chuo.

2. MAMBO YA MSINGI KWA WATUMISHI KUZINGATIA

1. Utoaji wa huduma bora kwa wadau wetu wakiwemo wanafunzi
2. Kufanya kazi kwa bidii, juhudi na maarifa, kuwa wabunifu, kujituma (kuwajibika)
3. Kuzingatia Maadili ya Utumishi wa umma- kufanya kazi kwa uadilifu, kuwahi kazini, kuwepo sehemu ya kazi muda wa kazi, mavazi nadhifu, mawasiliano yenye afya na viongozi wako, kuheshimu Mamlaka, mahusiano mazuri kazini, n.k
4. Kudhibiti uvujaji wa siri za Serikali/Taasisi, tuzingatie matumizi sahihi na salama ya mitandao ya kijamii.Tuitumie mitandao ya kijamii vizuri tusirushe taarifa isiyokuhusu au isiyo na maadili.
5. Tumia vyanzo sahihi kupata taarifa ili kujiridhisha kabla ya kusambaza katika mitandao ya jamii ili kuepusha upotoshwaji katika jamii.
6. Kuzingatia taratibu na miongozo katika kuwasilisha hoja/malalamiko/changamoto mbalimbali katika eneo lako la kazi.
7. Wakuu wa idara wafanye vikao kila mwezi ili kutoa fursa kwa watumishi kujadili mambo mbalimbali kwa ajili ya ustawi wa watumishi, idara, Chuo na Taifa kwa ujumla.

3. MAJIBU YA HOJA MBALIMBALI ZA WATUMISHI

3.1. Madai ya Malimbikizo ya mishahara

Hatua ya kwanza ya uhakiki wa malimbikizo ya mishahara imekamilika, watumishi wanaodai ni 92 (Wanataaluma 80 na waendeshaji 12). Fomu za madai yao zipo hatua ya pili ya uhakiki kwenye Kurugenzi ya Fedha na Mipango, zikikamilika zitawasilishwa kwa Mkaguzi wa ndani, na baadae zitawasilishwa kwenye Mamlaka za juu za Serikali kwa ajili ya kuombewa idhini ya malipo.

3.2 Mchakato wa Mpango wa Motisha (Incetive Scheme)

Taarifa ya kupitia Incetive Scheme tayari ilishawasilishwa na hatua inayofuata ni kuwasilisha kwenye Baraza la Wafanyakazi na kisha kwenye Bodi kwa ajili ya idhini na kuwasilishwa kwenye Mamlaka za juu za Serikali kwa ajili ya kuombewa idhini ya malipo.

3.3 Ruhusa ya watumishi kwenda masomoni

Kutokana na changamoto ya watumishi waliopo masomoni kuchelewa kumaliza masomo yao na kurudi kazini kumesababisha upungufu wa watumishi katika idara mbalimbali na kusababisha matumizi makubwa ya fedha za kuwalipa watumishi wa mkataba. Hivyo Bodi iliamua kuwa mwaka huu 2023 kustisha kwa muda kuruhusu watumishi kwenda masomoni hadi mwaka 2024 ili waliopo masomoni wamalize na mchakato wa ajira mpya unaoendelea ukamilike na idadi ya watumishi iongezeke.

3.4 Kukwama kwa malipo mbalimbali ya wanataaluma

Malipo ya posho mbalimbali kwa wanataaluma yatalipwa kulingana na mapato ya ndani ambayo yanategemea malipo ya ada za wanafunzi. Baadhi ya malipo hayo ni:

i. Malipo ya kufundisha masomo ya ziada (Extra module teaching);

ii. Malipo ya kusimamia mitihani ya mwisho wa muhula wa pili (Julai);
iii. Malipo ya maandalizi ya vikao vya matokeo kwa maafisa mitihani;
iv. Malipo ya vikao mbalimbali vya kupitisha matokeo;
vi. Malipo ya kusahihisha tafiti za wanafunzi;
vii. Malipo ya kusimamia mitihani ya supplementary na special.

3.5 Changamoto katika miundombinu ya kufundishia na kujifunzia

Licha ya ukweli kuwa kumekuwepo na maboresho makubwa katika miundo mbinu ya kufundishia/kujifunzia bado kuna changamaoto kadhaa zinazotakiwa kufanyiwa kazi. Baadhi yake ni: -

1) Kumbi zote za SAS 1-4 hazina hewa ya kutosha, hivyo kutenegeneza joto kali (ziwekewe feni);
2) Ukumbi wa Benjamini Mkapa umeme ukikatika, jenereta ama halisapoti au ukumbi wenyewe una shida;
3) Majengo ya kitivo cha FASI na EDUCATION kutounganishwa kwenye generator, hivyo umeme ukikatika majengo yote yanakuwa gizani na hivyo kukwamisha utendaji kazi wa wativa na Wakuu wa Idara.

3.6. Uteuzi wa mwakilishi wa MNMASA katika Bodi ya Chuo

Bodi ya Utawala ya Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, inatakiwa kuwa na wajumbe wafuatao:

1) Mwenyekiti ambaye anateuliwa na Rais
2) Mjumbe anayewakilisha Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia
3) Mjumbe anayewakilisha Wizara ya Fedha
4) Mjumbe anayewakilisha Baraza la Wafanyakazi la Chuo
5) Mjumbe anayemwakilisha Mwanasheria Mkuu wa Serikali

6) Mjumbe anayewakilisha Wanataaluma wa Chuo (MNMASA)
7) Mjumbe anayewakilisha Serikali ya Wanafunzi (MASO)
8) Mjumbe anayewakilisha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar
9) Mjumbe anayewakilisha Taasisi za elimu ya juu za Serikali

Mwenyekiti wa Bodi anateuliwa na Rais na wajumbe wa Bodi wanateuliwa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia. Hivyo, Majina ya viongozi wa MNMASA na MASO yalishawasilishwa kwenye mamlaka ya uteuzi, na mchakato bado unaendelea kwa mujibu wa taratibu za uteuzi.

3.6. Watumishi kukosa eneo la maegesho ya magari jirani na geti kuu

Chuo kimetenga maeneo mbalimbali kwa ajili ya maegesho ya magari katika sehemu mbalimbali za chuo, likiwepo eneo la maegesho ambalo lipo mbele ya ukumbi mpya wa mihadhara ambao upo karibu mita kama 100 kutoka gate kuu.

3.7. Waendeshaji waliofundisha hawajalipwa kwa kazi za ziada (extra duty)

Malipo yatalipwa kwa mujibu wa taratibu na miongozo iliyopo.

3.8. Watumishi wanazuiliwa kuhudhuria semina mbalimbali

Watumishi wanaruhusiwa kushiriki semina ila kulipia gharama za semina inategema Bajeti iliyotengwa kwa ajili ya mafunzo ya muda mfupi na mapato halisi katika Mwaka husika.

4. HITIMISHO

Kila mtumishi anatakiwa kutambua Dira ya Chuo ni kuwa kitovu cha utoaji wa Maarifa bora kwa kutoa Elimu na Mafunzo kuhusu ubunifu na Uvumbuzi na Kuendeleza Amani na Umoja wa Kitaifa.